
NEW LIFE
IN CHRIST

MAISHA MAPYA
NDANI YA KRISTO

DISCIPLESHIP SERIES I

FULL LIFE MINISTRY KENYA

NAME _____

Purpose: Provide teachings to equip the body of Christ to become warrior disciples of Jesus Christ. Since we are all living in the "Last Days" before the return of Jesus Christ, the command to "Go Make disciples...teaching them to observe all I have commanded you" is immediate.

Copyright © June 2014

Written By: Bishop Kenny Chivington - Full Life Ministry Kenya

Madhumuni: Kunatoa mafundisho ya kuimarisha mwili wa kristo ili uwe mashujaa wanafunzi wa Yesu Krito. Maana tunaishi katika siku za mwisho, kabla ya kurudi kwake Yesu Kristo, amri ya kwenda kuwafanya wanafunzi, kuwafundisha kushika yote tulioamriwa, ni ya dharura.

Hikimiliki © 06 2014

Mwandishi: Askofu Kenny Chivington – Full Life Ministry Kenya

INTRODUCTION

These next 12 lessons have been written, that you as a follower of Jesus Christ, will walk your New Life's journey learning who you are in the One who gave His life for you. Each lesson is a separate study in which you will learn Truth and then with each following lesson, build a foundation of Truth that cannot be shaken or destroyed by this present world.

Take whatever time you need to allow the Bible's Truth to become part of you. Memorizing the Truth will build your faith and prepare you to win the battles that lay ahead of you. Memory verses are at end of book.



You now are in a battle in which hell itself desires your defeat, but Jesus Christ has already secured your victory, if you will just obey Him.

“The thief (satan) comes to steal, kill and destroy, but I (Jesus) have come that they might have life and life more abundantly” John 10:10

Masomo yafuatayo kumi Na mbili, yameandikwa Ili wewe Kama mwanafunzi wa Yesu Kristo uweze kutembea safari ya maisha mapya, ukijifunza kwamba uko ndani ya yule aliyepeana maisha yake kwako.

Kila somo ni la kipekee ambapo uta jifunza ukweli halafu kwa kila somo linalufuata litajenga msingi wa ukweli ambao hauwezi kutingisika wala kuharibiwa na ulimwengu wa sasa. Kariri vifungu ambavyo vimewekwa mwisho wa kitabu hiki.



Sasa, uko katika vita ampapo kuzimu inatamani ushindwe. Lakini Yesu Kristo tayari amehifadi ushindi wako iwapo tu utatii

‘Mwizi [shetani] huja kuiba, kuuwa na kuharibu, bali Mimi [Yesu] nimekuja ili wawe na uzima kasha wawe nao tele.’Yohana10:10

The most important decision in your lifetime is to accept Jesus Christ as your personal savior. John 3:3 says “Except a man be born again, he cannot see the kingdom of God”. When you trusted Jesus to be your savior you were born again. Your new birth, by the Spirit of God has made you a new creature. II Cor. 5:17 says “If any man be in Christ, he is a new creature. Old things are passed away, behold all things are become new” Your old beliefs, your old attitudes, your old habits are beginning to pass away. The way you now view life is changing.

It is important to understand and review God’s plan of salvation. Why does anyone need salvation? Romans 3:23 says: “All have sinned and come short of the glory of God” Who has sinned? ALL. Next Romans 6:23 says “For the wages of sin is death, but the gift of God is eternal life through Jesus Christ” What wages do we get because we have sinned? DEATH Yes, eternal death which means eternal separation from God. How do we escape this death? We cannot do it ourselves. Titus 3:5 says “Not by works of righteousness which we have done, but according to His mercy He saved us” JESUS did it for us, on the cross. He took our punishment...our wages. I Peter 3:18 says “For Christ also hath once suffered for sins, the just for the unjust, that He might bring us to God, being put to death in the flesh, but quickened by the Spirit”

Questions: 1. Explain what decision have you made:

2. Explain words why have you made this decision:

Uamuzi wa muhimu sana katika maisha yako, ni kumkubali Yesu Kristo awe bwana na mwokozi wa maisha yako. Yohana 3:3 inasema, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuona ufalme wa mbinguni. Ulipomuamini Yesu awe mwokozi wako, ulizaliwa mara ya pili. Kuzaliwa kwako upya kwa roho wa Mungu, umefanyika kiumbe kipya. Wakorintho wa pili 5:17 inasema, ”mtu akiwa ndani ya Kristo amefanyika kuwa kiumbe kipya, ya kale yote yamepita tazama yote sasa yamefanyika kuwa mapya ”Imani yako ya kale, mtazamo wako wa kale, tabia yako ya kale yote yanaanza kupita. Jinsi unavyotazama maisha inaanza kubadilika.

Ni muhimu kuelewa na kutafakari tena mpango wa Mungu wa wokovu. Ni kwa nini kila mtu anahitaji wokovu? Warumi 3:23 inasema ”Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa mungu” Nani ametenda dhambi? WOTE Kisha Warumi 6:23 inasema ”Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele kupitia kwa Yesu Kristo” Tunapata mshahara gani kwa sababu tumetenda dhambi? MAUTI ndiyo, mauti ya milele ambayo inamaanisha kutenganishwa milele na Mungu. Twaazaje kuepuka haya mauti? Hatuwezi kufanya hivyo sisi wenyewe. Tito3:5 inasema ”Si kwa matendo ya haki ambayo tumetenda bali kwa huruma zake tumeokolewa” YESU alitufanyia hayo pale msalabani. Alichukua adhabu zetu...Mshahara wetu Petero wa kwanza 3:18 inasema”Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa ”

Maswali: 1. Eleza kwa maneno yako mwenyewe umefanya uamuzi gani:

2. Eleza kwa maneno yako mwenyewe ni kwa nini umefanya uamuzi huu:

What is our part for God’s plan? First, to **BELIEVE** (to place our trust) in Jesus Christ. Acts 16:31 says “Believe on the Lord Jesus Christ and thou shall be saved.” Next, **CONFESS** Jesus is your Lord. Romans 10:9 says “If thou shalt confess with thy mouth the Lord Jesus and shalt believe in thine heart that God hath raised Him from the dead, thou shalt be saved.” And then **REPENT** (turn away from your sins) In Luke 13:3 Jesus said “**Except ye repent**, ye shall all likewise perish.” Turn away from your past ways of sinning and start to follow the teachings of Jesus. You ask “How do I do that?”

Let’s look at one way you can start to do that. II Timothy 2:15 says “Study to shew thyself approved unto God, a workman that needeth not to be ashamed, rightly dividing the Word of Truth.” Study...Study does not only mean to read. It means to find out what you are reading means to you and then do it. James 1:22 says “But be ye doers of the Word and not hearers only”. **Do what it says ?**

You may ask how can I keep from sinning? King David tells you how in Psalms 119:9-11 “Wherewith shall a young man cleanse his way? By taking heed thereto according, to thy Word. With my whole heart have I sought thee. Oh let me not wonder from thy commandments. **Thy Word have I hid in mine heart** that I might not sin against Thee.” He said to put the Word of God in your heart...The Word will keep you, if you will keep it. Again, how do you do that? You put it inside you, in your heart. So that even if you do not have a Bible, you have it. You put it inside you, in your heart. So that even if you have a Bible, but someone takes it away from you, you still have it. You commit it to memory.

Questions: 1. Why do I desire to repent?

2. From what I read in this lesson, how am I to follow Jesus?

Sehemu yetu ni ipi katika mpango wa Mungu? Kwanza, **KUAMINI** (kuweka tumaini letu) ndani ya Yesu Kristo. Matendo ya mitume 16:31 inasema ”amini bwana Yesu kristo nawe utaokoka” Kisha **UKIRI** Yesu kuwa bwana. Warumi 10:9 inasema ” kwa sababu ukikiri kwa kinywa chako kuwa Yesu ni bwana nauamini moyoni mwako kuwa Mungu alimfufua kutoka katika wafu utaokoka”. Kisha **TUBU** (ugeuke uache dhambi zako). Katika Luka 13:3 Yesu alisema ” Nawaambia, sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.” Geuka kutoka kwa dhambi, njia za kale za dhambi na uanze kufuata mafundisho ya Yesu. “Unauliza ninafanaje hivyo?”

Wacha tuangalie njia moja jinsi ambavyo waweza kuanza kufanya hivyo. Timotheo wa pili 2:15 inasema ”jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli”, Kujitahidi kusoma haimaanishi kusoma tu, bali inamaanisha kutafakari yale maandiko yanamaanisha kwako. Yakobo 1:22 inasema ”Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikilizaji tu”. Tendeni jinsi inavyosema.

Waweza kuuliza, nawezaje kujiepusha na kutenda dhambi? Mfalme Daudi anakueleza ni jinsi gani katika Zaburi 119:9-11 ”Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata neno lako. Kwa moyo wangu wote nimekutafuta, Usiache nipotee mbali na maagizo yako. Moyoni mwangu nimeliweka neno lako. Nisije nikakutenda dhambi.” Amesema nilificha neno lako moyoni mwangu... neno litakuweka kama utaliweka moyoni. Tena utafanyaje hivyo? Kuliweka ndani mwako, ndani ya moyo wako, ili kwamba hata kama huna biblia unalo neno. Ili kwamba hata kama mtu ataichukua biblia yako, bado utakuwa unalo neno, liweke katika tafakari yako.

Maswali: 1. Kwa nini natamani kutubu?

2. Kutoka Kwa yale umejifunza katika somo hili, ni ipi njia moja ya kumfuata Yesu.

Let's take a little deeper look at the book you are going to study, called the Bible. The Bible is a book of books. Sixty-six separate books divided into the New Testament & Old Testament. We will learn later in another lesson why we have both a New & an Old Testament. In the book of Saint John Chapter 1 verses 1 & 2 "In the beginning was the Word, and the Word was with God, and the Word was God. The same was in the beginning with God." We learn here that this book is different from any other book ever written.

We will examine just a few things that this book offers to anyone who will open its pages and study what God Himself declares to those who have placed their trust in Him. Philippians 1:6 says, "Being confident of this very thing, that He which has begun a good work in you will perform it until the day of Jesus Christ" That is a promise that God is going to continue working in your life from now on. Phil. 4:19 says "But my God shall supply all your need according to His riches in glory by Christ Jesus" God has promised to meet all that you need. Phil. 4:6-7 says, "Be careful for nothing, but in everything by prayer and supplication with thanksgiving let your requests be known unto God. And the peace of God, which passeth all understanding shall keep your hearts and minds through Christ Jesus." God has promised peace to you in all and every situation.

Questions: 1. Where was the Word in the beginning?

2. What promise above means a lot to you and explain why?

Wacha tukitazame kiundani kitabu tunachoenda kujifunza kinachoitwa Biblia. Biblia ni kitabu cha vitabu. Vitabu tafauti sitini na sita ambavyo vimegawanywa katika makundi mawili, agano jipya na agano la kale. Katika kitabu cha Yohana mtakatifu 1:1 na mbili, ”hapo mwanzo kulikuweco neno,naye neno alikuweco na Mungu naye alikuwa Mungu”. Neno hili lilikuwapo na Mungu. Tunajifunza hapa ya kwamba Kitabu hiki ni tufauti na vitabu vingine ambavyo vimewahi kuandikwa.

Tutatazama vitu vichache ambavyo kitabu hiki kinapeana kwa yeyote anayefungua kurasa zake na kujifunza yale Mungu ameamuru kwa wote ambao wameweka tumaini lao kwake. Wafilipi 1:6 inasema ”basi nina hakika kwamba Mungu aliyeanza kazi hii njema ndani yenu, ataindeleza hadi ikamilike hadi siku ile ya kristo Yesu”. Hii ni ahadi ambayo Mungu ataendelea kuitimiza maishani mwako tangu sasa na kuendelea. Wafilipi 4:19 inasema ”Lakini Mungu wangu atakutana na mahitaji yenu kulingana na utajiri wake katika utukufu katika Kristo Yesu”. Mungu amehaidi kukutana na mahitaji yako yote. Wafilipi 4:6-7 inasema ”Usijisumbue kwa neno lolote, bali katika kila jambo, kwa kusali na kuomba na shukrani, fanyeni mahitaji yenu yajulikane na mungu. Na amani ya Mungu ipitayo akili zote za wanadamu itahifadhi salama mioyo na akili yenu katika katika Kristo Yesu.”. Mungu amekuhaidi amani katika hali zote.

Maswali: 1. Neno lilikuwa wapi mwanzo?

2. Ni ahadi zipi hapo juu ambazo zinamaana sana kwako na kwa nini?

Prayer... This word has taken on many forms and rituals in the past as well as today. Many are not biblical and some are even evil. We will look at what the Bible has to say about this essential part of your new life in Christ.

First of all we see God commands us to pray. Luke 18:1 says “And he (Jesus) spake a parable unto them to this end, that men ought always to pray, and not to faint.” Then, 1 Thess. 5:17 says “Pray without ceasing” You may say I will never be able to do that. Actually, yes you can, if you so desire. Prayer is the continual turning of our hearts to God about everything we need or desire until your subconscious mind is continually in touch with God.

John 15:7 says “If you abide in me and my words abide in you, ye shall ask what ye will and it shall be done unto you.” Then James tells us in Chapter 4 verse 3 “Ye ask and receive not, because ye ask amiss, that ye may consume it upon your lusts.” God knows the intent of our hearts before we ask, so our hearts must be in alignment with His will. And as you read (study) His Word your heart will grow towards Him as you learn and line up with His Word.

Questions: 1. How important is it to pray? Explain.

2. Describe how much you should pray?

Maombi...Hili ni neno ambalo limechukua mitindo Na desturi nyingi siku zilizopita na hata sasa. Nyingi yazo si za kibiblia na nyingine hata ni za kishetani. Tutazame biblia inavyosema kuhusu sehemu hii **muhimu** katika maisha yako mapya ndani ya Kristo.

Kwanza kabisa katika yote tunaona Mungu **akituamuru** kuomba. Luka 18:1 inasema “Naye (Yesu) aliwasimulia mfano kuonyesha kwamba ni lazima kusali daima bila kukata tamaa”. Kisha Wathesolonike wa kwanza 5:17 inasema ”ombeni bila kukoma” Waweza kusema siwezi fanya hivyo, hakika waweza iwapo wataka. Maombi ni hali ya kuendelea kugeuza mioyo yetu na kumuelekea Mungu kuhusu yote unayohitaji hadi mawazo yako yashikamane kabisa na Mungu.

Yohana 15:7 inasema ”Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu, yakikaa ndani yenu ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa”. Kisha yakobo anatuambia katika mlango wa 4 na mstari wa tatu kwamba ”Tena mkiomba hampati kwa sababu mnaomba kwa nia mbaya; mnaomba ili mpate kutosheleza tamaa zenu”. Mungu anajua makusudi ya mioyo yetu kabla hatujaomba, kwa hivyo mioyo yetu inapaswa kuambatana na mapenzi ya mungu. Unapolisoma neno la Mungu, moyo wako takuwa kumuelekea Mungu unapojifunza na kuwa sawasawa na neno lake.

Maswali: 1. Ni muhimu jinsi gani kuomba? Eleza.

2. Elezea unahitaji kuomba kwa kiasi gani?

Last lesson we learn the importance of prayer. Now let's look at how we should pray. In the 6th chapter of Matthew, Jesus says much about how we should pray. Verses 5 & 6 tell us not to pray for the reason to be seen or heard by men, but that much of our praying is to be done alone with God. Verses 7 & 8 say not to use repetition to make your prayers long, just pray what is in your heart and mean what you pray.

Looking into verses 9 – 13 we are instructed to honor God when we pray, ask for our daily needs, ask forgiveness for our sins and empower us to live free from satan. And then verses 14 & 15, we learn that we **MUST FORGIVE OTHERS** if we are to be forgiven. Jesus was telling us to talk to God about everything. That being said, you have much to pray each and every day. Prayer is a habit, a way of life that only you can make happen.

If you have not started to have an alone time with God in prayer, then start today. As you talk with Him each day, it will become a “normal” part of your daily life. Prayer, as you practice it, will allow you to become more acquainted with the One who gave His Son so that you would be able to enjoy fellowship with Him eternally.

Questions: 1. Explain what are 3 things we should pray?

2. How often should you pray? Explain.

Somo lililopita, tulijifunza kuhusu umuhimu wa maombi. Sasa wacha tuangalie jinsi gani tunapaswa kuomba. Katika mathayo 6 :5 na 6 inatambia tusiombe ili kuonekana na kusikika na watu, bali maombi yetu mengi yafanywe tukiwa peke yetu na Mungu, vifungu vya 7 na 8 vinasema tusiombe kwa kujirudia rudia ili kufanya maombi yetu kuwa marefu. Omba yaliyo moyoni mwako na maanisha unayoomba.

Tukitazama vifungu vya 9 hadi 13 tunaangizwa kumtii Mungu tunapoomba, omba mahitaji yako ya kila siku, omba msamaha wa dhambi zetu, na kutiwa nguvu za kuishi maisha ya uhuru na kushinda shetani. Kisha vifungu vya 14 na 15 tunajifunza kwamba LAZIMA TUSAMEHE WENGINE iwapo twahitaji kusamehewa. Yesu alikuwa anatwambia tuzungumze naye juu ya kila kitu katika maombi, baada ya kusema hayo twafahamu ya kwamba tuna mengi ya kuzungumza na Mungu kila siku. Maombi ni desturi, hali ya maisha ambayo wewe waweza kuifanya.

Kama haujaanza kuwa na muda wa pekee wa kuwa na Mungu katika maombi, basi anza leo. Utakapoongea naye kila siku katika maombi, basi itakuwa sehemu ya kawaida ya maisha yako ya kila siku. Jinsi utakavyoweka katika mazoezi maombi, itakuwezesha kujifahamisha vyema na Yule aliyemtoa mwanawake ili ufurahie ushirika naye milele.

Maswali: 1. Eleza ni mambo yapi matatu ambayo wapaswa kuyaomba?

2. Wahitaji kuomba mara ngapi? Eleza.

Fellowship is very important. In your new life with Christ the people you spend time with will affect your Christian walk. Either for good or bad. God saw that this fellowship is vital in our growth toward maturity in Christ. He says in Hebrews 10:24-25 “Let us consider one another to provoke unto love and good works; Not forsaking the assembling of ourselves together as the manner of some is, but exhorting one another and so much the more as ye see the day approaching.”

As Christian brothers and sisters, we are to encourage one another to follow Christ’s teachings. Also there is strength in fellowship. The bible says in Matt. 18:20 “For where two or three are gathered together in my name; there I am in the midst of them.” We do to some extent become like those we fellowship with. At our place of work or at our school, we can be lights in a sometimes dark place by living a Christ-like life through our words and deeds. We need then to come back into fellowship with other Christians to gain encouragement and strength.

Questions: 1. Why is it important to fellowship with other Christians?

2. Are you able to fellowship with other Christians? Explain

Ushirika ni muhimu sana. Katika maisha yako mapya na Kristo, watu unao shirikiana nao wataathiri ukristo wako, Katika uzuri au katika ubaya. Mungu aliona kwamba ushirika ni muhimu katika kukuwa kwetu kuelekea ukomavu katika Kristo. Anasema katika Waebrania 10:24-25 “Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; Wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia”

Kama ndugu na dada, tunahitaji kuhimizana kufuata mafundisho ya Kristo. Pia kuna nguvu katika ushirika. Biblia inasema katika Mathayo 18: 20 ”Walipo wawili au watatu wamekusanyika katika jina langu, mimi nipo katikati yao”. Kwa kiasi Fulani sisi huwa kama wale tunaoshiriki nao. Mahali petu pa kazi au shuleni, twaweza kuwa nuru wakati mwingine katika giza kwa kuishi maisha ya kikristo katika maneno na matendo yetu. Tunahitaji basi kurejelea ushirika na wakristo wengine kupata kutiwa moyo na nguvu.

Maswali: 1. Mbona ni muhimu kuwa na ushirika na wakristo wengine?

2. Je waweza kuwa na ushirika na wakristo wengine? Eleza

The Holy Spirit – Who He is...

The Holy Spirit is God, and has equality with the Father & the Son. He is not an “it” or an “influence”. He is God, the Holy Spirit, and is set forth in the Bible as being distinct from the Father and the Son. (Matthew 28:19)

The Holy Spirit was actively engaged in the creation as described in the 1st chapter of Genesis. Verse 2 says “the Spirit of God moved upon the face of the waters.” He was active in the lives of men in the Old Testament like king Saul. “The Spirit of the Lord will come upon thee.” I Samuel 10:6 He is active today as described in John 14:26 “The Comforter, which is the Holy Spirit, whom the Father will send in my name, He shall teach you all things and bring all things to your remembrance” In the original text, the word Comforter means: One of the same likeness & One who comes along side of. He comes into our lives to lead & guide us.

Questions: 1. Explain who is the Holy Spirit?

2. Is the Holy Spirit our comforter? Explain.

Roho Mtakatifu-Yeye ni nani

Roho Mtakatifu ni Mungu, naye ni sawa na baba na mwana. Yeye si kitu au nguvu Fulani. Yeye ni Mungu, Roho Mtakatifu naye anaelezwa katika biblia kama Mungu kibinafsi kando na Mungu baba na Mungu mwana. (Mathayo 28:19)

Roho Mtakatifu alishiriki katika uumbaji jinsi inavyoelezea katika Mwanzo 1:2 ambapo inasema "Dunia ilikuwa bila umbo na tupu. Giza ilikuwa imefunika vilindi vya maji, na Roho ya Mungu ilikuwa ikitanda juu ya maji." Alikuwa akitenda kazi katika maisha ya watu katika agano la kale kama mfalme Sauli. "Roho wa Bwana atakuja juu yako". Samweli wa kwanza 10:6. Yeye yuatenda kazi hata leo kama inavyoelezwa katika Yohana 14:26. Mfariji ambaye ni Roho Mtakatifu ambaye baba atamtuma katika jina langu, atawafunza yote, na kuwakumbusha yote, katika maandiko asili mfariji yamaanisha Yule ambaye anafanana na, Yule ajaye kando ya. Yeye huja maishani mwetu kutuongoza na kutuelekeza .

Maswali: 1.Elezea Roho Mtakatifu ni nani?

2. Je Roho Mtakatifu ni mfariji? Eleza.

The Holy Spirit – What He does

The Holy Spirit helps us to obey the Truth. I Peter 1:22 “Seeing ye have purified your souls in obeying the truth through the Spirit unto unfeigned love of the brethren, see that ye love one another with a pure heart fervently” He directs us to not walk after the flesh. Galatians 5:16 “Walk in the Spirit and ye shall not fulfill the lust of the flesh” He leads us as we are now children of God.

Romans 8:14&16 “For as many as are led by the Spirit of God, they are the sons of God. The Spirit itself beareth witness with our spirit, that we are the children of God.” The Holy Spirit enables us to live our life for Jesus and not just serve our flesh. Romans 8:13 “For if ye live after the flesh, ye shall die: but if ye through the Spirit do mortify the deeds of the body, ye shall live.” He helps us to pray.

Romans 8:26 “Likewise the Spirit also helpeth our infirmities: for we know not what we should pray for as we ought: but the Spirit itself maketh intercession for us with groanings which cannot be uttered.” He gives us liberty – freedom .

II Cor. 3:17 “Now the Lord is that Spirit: and where the Spirit of the Lord is, there is liberty.”

Questions: 1. Explain how the Holy Spirit helps us live for Jesus?

2. What does He do in our lives today?

Roho Mtakatifu-Kazi yake

Roho Mtakatifu anatusaidia kutii ukweli. petero wa kwanza 1:22 “mkiisha takaswa nafsi zenu kwa kutii ukweli kupitia kwa Roho Mtakaifu kupitia kwa upendano wa wandugu, kwa upendano wa ndugu usio na unafiki, bali kwa usafi wa moyo. Anatauelekeza kuwa tusitembee katika mwili” tembea katika roho nawe hautatimiza tamaa za mwili”. Wagalatia 5:16 anatuongoza maana sasa sisi ni watoto wa Mungu” kwa maana jinsi wengi wanaongozwa na roho mtakatifu, wao ni wana wa Mungu. Roho mwenyewe anashuhudia roho zetu kwamba sisi ni watoto wa mungu. Warumi 8:14 na 16. Roho Mtakatifu anatuwezesha kumuishia Kristo na sio kutumikia mwili wetu.” Kwa maana tukiishi katika mwili tutangaamia bali tukiishi katika roho na sio kwa miili yetu, tutaishi” Warumi 8:13. Yeye hutusaidia katika kuomba, pia Roho Mtakatifu hutusaidia katika udhaifu: kwa maana hatujui jinsi inavyotupasa kuomba, bali roho mtakatifu mwenyewe hutuomba kwa Mungu kwa mlio usioweza kuelezwa.” Warumi 8:26. Anatupa uhuru.”Sasa bwana ni roho na palipo roho wa bwana kuna uhuru.“ Wakorintho wa pili 3:17

Maswali: 1. Elezea jinsi Roho Mtakatifu anatusaidia kumuishia Yesu.

2. Yeye anafanya nini maishani mwetu Leo?

Faith – A Word or a Lifestyle

Let's examine what Faith is. According to Hebrews 11:1 "Now faith is the substance of things hoped for, the evidence of things not seen" faith has substance. It is something that is real not just some magical mist in the air. So let's look at faith through the window of what has happened to you...your New Life in Christ. You have trusted, placed your faith in Christ for your "New Life." Galatians 2:20 sums up what placing your faith in Christ (the substance) has done for you as well as the rest of your journey until you meet Jesus face to face in eternity. It says "I have been crucified with Christ: nevertheless I live yet not I, but Christ who lives in me; and the life I now live in the flesh I live by faith in the Son of God, who loved me and gave Himself for me."

You are already exercising your faith by placing your trust in what Christ did for you on the cross. And now you continue to do the same, placing your trust, your faith to live this new life...a new lifestyle. Christ now lives inside of you, never to leave, but always to enable you to live for Him. How exciting it is to know that Christ lives inside of you! (The evidence) is what others see and will continue to see in you as Christ demonstrates Himself to others through your life.

Questions: 1. Will you be alone in this New Life? Explain.

2. Is Faith just a word? Explain.

Imani-ni neno au hali ya maisha

Wacha tutazame imani ni nini. Kulingana na Waebrania 11:1 ”kuwa na imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, kuamini kabisa mambo tusingiyoyaona” imani yaweza kuguswa. Imani ni kitu cha kweli si uganga katika hewa. Kwa hivyo wacha tuangalie imani kupitia kwa dirisha la yale yaliokutendekeka... maisha yako mapya ndani ya Kristo. Umetumaini, umeweka imani yako kwa Kristo kwa maisha yako Wagalatia 2:20 inaelezea kile kuweka imani yako ndani ya Kristo imefanya kwako na kwa safari yako hadi utakapokutana na Kristo macho kwa macho katika umilele. Inasema ”nimesulubiwa na Kristo, si mimi ninaeishi sasa bali kristo anaishi ndani yangu; maisha ninayoishi sasa katika mwili ninaishi kwa imani katika mwana wa Mungu, ambaye alinipenda na akajitoa mwenyewe kwa ajili yangu.

Tayari unaweka imani yako katika mazoezi kwa kutumainia yale Kristo alifanya kwa niaba yako pale msalabani. Hivyo unaendelea kufanya hivyo, ukiweka tumaini lako, na imani yako kuendelea kuishi haya maisha mapya... maisha mapya, Kristo sasa anaishi ndani yako na kamwe asikuwache bali daima kukuwezesha kumuishia. Inasisimua jinsi gani kufahamu kwamba Kristo anaishi ndani mwako (ushahidi) ni kile wengine watakiona na kuendelea kuona ndani mwako, Kristo akijidhihirisha kwa wengine kupitia kwa maisha yako.

Maswali: 1. Je utakuwa peke yako katika maisha mapya? Eleza.

2. Je imani ni neneo tu? Eleza.

To Serve & Obey Jesus

Christ came to serve...Mark 10:45 “For even the Son of man came not to be ministered unto, but to minister and give His life a ransom for many.” He is our example to follow and we will encounter trials along the way. You must put Jesus first in your life. Jesus tells us “If anyman will come after me, let him deny himself, take up his cross daily and follow me.” Luke 9:23 Then, in Romans 12:1 we are instructed “I beseech you therefore brethren, by the mercies of God, that ye present your bodies a living sacrifice, holy, acceptable unto God.” We have been give a great opportunity to show others...Jesus. The writer of Romans instructs us “And be not conformed to this world, but be ye transformed by the renewing of your mind, that you may prove what is that good and acceptable and perfect will of God”. Romans 12:2

Serving Jesus is equal to obeying Jesus. He lived a life not conformed to this world. He was an outcast because He would not bend to it rule. We must do the same as the world tries to entice us to its ways. We again receive instruction from the book of I John 2:15-16 “Love not the world, neither the things that are in the world. If anyman loves the world, the love of the Father is not in him. For all that is in the world, the lust of the flesh and the lust of the eyes and the pride of life, is not of the Father, but is of the world.” You are not of this world any longer. You have been purchased by the blood of Jesus and you are now His servant. His servant to serve a lost and dying world that is filled with real people that will either spend eternity with Christ or eternity without Him in hell. You now have a message to deliver.

Questions: 1. How are you to live your life now that is different than before?

2. Do you believe that Jesus desires your obedience? Explain.

Kutumika na kumutii Yesu

Kristo alikuja kutumika...Marko10:45 "Maana mwana wa adamu hakuja kutumikiwa, ila kutumika na kutoa maisha yake kama fidia kwa watu wengi". Yeye ni mfano wetu wa kufuata na tutakutana na majaribu katika safari hii. Lazima umuweke Yesu awe wa kwanza katika maisha yako. Yesu anatuambia "yeyote anayetaka kunifuata lazima ajikane nafsi yake mwenyewe, ajitwike msalaba wake mwenyewe na anifuata". Luka 9:23 Kisha Warumi 12:1 tunaagizwa 'ninawasihi wapendwa kwa huruma zake mungu, itoeni miili yetu kama dhabihu iliyohai takatifu na inayokubalika kwa Mungu" Tumepewa fursa ya kuwaonyesha wengine ...Yesu. Muandishi wa Warumi anatuagiza " Wala msiifuatishie namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu". Warumi 12:2

Kumtumikia Yesu ni sawa na kumtiii Yesu. Aliishi maisha yasiyokuwa ya starehe katika uliwengu huu. Alikataliwa kwa sababu hakukubaliana na sheria ya dunia hii. Hatupaswi kufanya jinsi uliwengu unavyofanya na kujaribu kutufunga. Katika njia zake. Pia tunapokea maagizo kutoka kwa waraka wa kwanza wa Yohana 2:15-16 "Musipende ulimwengu, wala vitu vilivyomo. Yeyote anayependa ulimwengu, kumpenda Mungu hakumo ndani yake. Yote yaliyomo ulimweguni,tamaa ya mwili ,tamaa ya macho na kiburi cha uzima, haitokani na mungu bali kwa ulimwengu." Ninyi si wa ulimwengu huu tena, mumenunuliwa kwa damu ya dhamani ya Yesu nawe sasa ni mtumishi wake. Mtumishi wake kutumikia ulimwengu uliopotea na unaokufa ambao umejaa watu ambao wataishi milele na Kristo au kuzimu bila yeye milele. Sasa unajumbe wa kupeana.

Mawali: 1.Wastahili kuishi aje maisha yako mapya maana sasa ni tafauti na awali?

2. Je unaamini kwamba Yesu anahitaji wewe umtii? Eleza.

Sharing Jesus

It is amazing that the God of the universe has chosen each of us to share His message to the world. Most of us will not become missionaries to other nations, but we are missionaries to those we live with & work with. Those people that you spend time with everyday or those that you may just talk to in passing. What a privilege...what a responsibility. Jesus gave each of us a commission “Go therefore and teach (make disciples) of all nations baptizing them in the name of the Father, the Son and the Holy Spirit, teaching them to observe all things I have commanded you” Matthew 28:19-20 You may say well I cannot do that. Well that is where God the Father has sent His Holy Spirit to equip us to do what He asks us to do. “But you shall receive power after that the Holy Ghost is come upon you and you shall be my witnesses unto me both in Jerusalem, and in all Judea and in Samaria and unto the uttermost part of the earth.” Acts 1:8 God has given you the power through the Holy Spirit to share Jesus with whoever comes in your path. Sharing what Jesus has done in your life is just sharing the truth that you personally have experienced.

Yes, God has called you to a high calling...sharing His Son with others. Yes, He has given you power to do what He asks. Yes, you will share Jesus to many. Some will accept and some will reject Jesus. That’s ok...Jesus said it would be that way. He only asks us to offer what He has offered to you. Again, you have been given the greatest opportunity ever offered to man. Sharing the Good News that Jesus came to this earth to give life to a dying world. You personally will make the difference in the lives of many of where they will spend eternity. The same words that Jesus told His disciples we speak now... **GO; GO INTO THE ENTIRE WORLD...**

Questions: 1. Does Jesus want you to share Him with others? Explain.

2. Who will help you to share Jesus with others?

Kushiriki Yesu Na wengine

Inashangaza kwamba Mungu amechagua kila mmoja wetu kushiriki ujumbe wake na ulimwengu. Wengi wetu hatuwezi kuwa wamishionari katika mataifa mengine bali sisi ni wamishoni kwa wale tunaishi na kufanya kazi nao. Wale watu ambao wewe huwa nao muda mwingi kila siku au wale wewe huwazungumzia ukipita. Ni fursa ya namna gani, ni majukumu ya namna gani ambayo tumepewa. Yesu alitupa mwito wetu “enendeni muwafanye wanafunzi katika mataifa yote, mukiwabatiza katika jina la baba, na mwana na Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kushika yote niliyowaamuru” Mathayo 28:19-20. Waweza kusema, Mimi siwezi kufanya hivyo. Hapo ndipo mungu baba amemtuma roho wake mtakatifu kutuimarisha kufanya yale ambayo anatuuliza kufanya. ”Nanyi mtapokea nguvu atakapowajia Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na Uyahudi wote, na Samaria na hata ulimwengu wote” Matendo ya mitume 1:18. Mungu amekupa nguvu kupitia kwa Roho Mtakatifu, kushiriki Yesu na yeyote tunayekutana naye. Kushiriki yale Yesu ametenda maishani mwako, ni kushiriki kibinafsi yale umeshuhudia

Ndio, Mungu amewaita katika mwito mkuu...kushiriki juu ya mwanawe na wengine, amekupa mamlaka kufanya yale amekuagiza. Ndio utashiriki Yesu kwa wengi, wengine watakubali na wengine watamkataa Yesu, hivyo ni sawa...Yesu alisema itakuwa hivyo. Anakuuliza tu upeane kile ambacho amekupa. Tena umepewa fursa kuu ambayo imewahi peanwa kwa mwanadamu. Kushiriki habari njema kwamba Yesu alikuja katika ulimwengu huu kupeana uzima kwa ulimwengu unaokufa. Binafsi utasababisha utafauti katika maisha ya wengi ambao wataishi milelele. Maneno yayo hayo yalisemwa na Yesu kwa wanafunzi wake, ambayo tunayanena sasa...ENENDA KATIKA ULIMWENGU WOTE...

Mwasali: 1. Je Yesu anataka ushiriki juu yake na wengine? Eleza.

2. Nani atakusaidia kushiriki juu ya Yesu na wengine?

Putting it all together

Having made your decision to follow Christ you are being transformed day by day to be more like Him. II Cor. 5:17 Studying the Bible each day will enable you to become a doer of the Word. James 1:22 When you are faced with a decision now, your 1st choice needs to be how do I pray about this and what does the Bible say about it. Using the Bible will bring peace as you continue to live in this world that is really a mess. Phil. 4:6-7 As you pray each day, ask God to draw you near to Himself. God the father wants to have fellowship with you every day. You are not limited as to how much time you can spend with Him because He is always available. Just like any other relationship, alone time together with Christ is so important. You will find that many things will compete for this intimate time. Only you can make those times happen. As you do you will find a deep desire to have more and more time with Christ.

You are never alone now and God has sent His Holy Spirit to walk with you and teach you. Galatians 5:16 Listen as He instructs with a small voice. He will only lead you where He desires for you to go. Yes it is a walk of faith, but that is now how you live. Galatians 2:20 - A life of service for the King of Kings. No greater honor lies here on this earth then to serve Him. It is a sacrifice, but the rewards are immeasurable and not of this world. Rom.12:1

God has chosen you to share His amazing gift of eternal life with anyone you may come in contact with. He will guide you, He will direct you and He will empower you to do beyond your wildest dreams. Why? Because He loves you. John 3:16 **Welcome to the family of God. Welcome to the fellowship of Believers. Welcome to the Father's arms!!!**

Questions: 1. Describe your life before trusting Jesus to be your Saviour?

2. Describe your life since you trusted Jesus to be your saviour?

Kuweka yote pamoja

Baada ya kufanya uamuzi wa kumufwata Kristo, unabadilishwa siku baada ya siku kuwa kama Kristo. Wakorintho wa pili 5:17, kujifunza biblia kila siku, itakuwezesha kuwa mtendaji wa neno. Yakobo 1:22 ukiwa umekabiliwa na uamuzi sasa, uchaguzi wako wa kwanza utakuwa; niombeje juu ya hili, na biblia inasema nini juu ya hili. Kutumia biblia itakuletea amani unapoendelea kuishi katika ulimwengu huu ambao umechanganyikiwa. Wafilipi 4:6-7 unapomba kila siku, muulize Mungu akuvute karibu naye. Mungu baba anataka kuwa na ushirika nawe kila siku. Haujapewa muda ambao anahitaji kuwa na mungu kwa sababu yeye anapatikana wakati wote. Kama vile katika uhusiano wowote ule, muda wa kuwa pekee na Kristo ni muhimu. Utapata kwamba mambo mengi yata gania muda huu wa kibinafsi kuwa na Kristo. Wewe tu ndio unaweza kufanya haya yatendeke, na unapofanya hivi utahisi shauku ya kindani ya kuwa na muda mwingi zaidi wa kuwa na Kristo.

Wewe hauko peke yako sasa na Mungu ametuma Roho wake Mtakatifu kutembea nawe na kukufundisha. Wagalatia 5: 16. Sikiza anapokupa maagizo na sauti ya upole. Yeye atakuongoza kule tu anataka uenda. Ndio ni safari ya imani, lakini hivyo ndivyo unavyoishi. Wagalatia 2:20 maisha ya huduma kwa mfalme wa wafalme. Hakuna heshima kubwa hapa duniani kama kando na kumtumikia. Ni kujitolea, lakini dhawabu ni maradhufu nayo si ya dunia hii. Warumi 12:1

Mungu amekuchagua kushiriki zawadi yake ya ajabu na yeyote ambaye utakutana naye. Atakuongoza, atakuelekeza naye atukupa nguvu kufanya zaidi ya ndoto zako. Kwa nini? Kwa sababu anakupenda Yohana 3:16 *Karibu katika jamii ya Mungu. Karibu katika ushirika wa waumini. Karibu katika mikono ya baba!!!*

Maswali: 1. Elezea maisha yako kabla ya kumuamini Yesu kuwa mwokozi wako?

2. Elezea maisha yako tangu umuamini yesu kuwa mwokozi wako?

MEMORY VERSES FOR LESSONS

30

Lesson 1 – Romans 6:23

Lesson 2 – II Corinthians 5:17

Lesson 3 – Philippians 4:19

Lesson 4 – Philippians 4:6-7

Lesson 5 – John 15:7

Lesson 6 – Romans 3:23

Somo la Kwanza – Warumi 6:23

Somo la Pili – Wakorintho wa pili 5:17

Somo la Tatu – Wafilipi 4:19

Somo la Nne – Wafilipi 4:6-7

Somo la Tano – Yohana 15:7

Somo la Sita – Warumi 3:23

MEMORY VERSES FOR LESSONS

Lesson 7 – Romans 12:1

Lesson 8 – Romans 12:2

Lesson 9 – Galatians 2:20

Lesson 10 – I John 2:15-16

Lesson 11 – Acts 1:8

Lesson 12 – I John 5:13

Somo la Saba – Warumi 12:1

Somo la Nana – Warumi 12:2

Somo la Tisa – Wagalatia 2:20

Somo la Kumi – Waraka wa kwanza wa Yohana 2:15-16

Somo la Kumi na Moja – Matendo ya Mitume 1:8

Somo la Kumi na Mbili – Waraka wa kwanza wa Yohana 5:13

These lessons can be copied and distributed *free of charge* in their original format for the making and building up of disciples of Jesus Christ.

Jesus Christ has already paid in full your sin debt.

Masomo haya yanaweza kunakiliwa na kusambazwa bure bila malipo katika hali yake ya awali kwa ajili ya kufanya na kujengo wanafunzi wa Yesu Kristo.

Kristo Yesu tayari amelipa deni ya dhambi zenu.